Toleo 79 - Muharram 1445 H / Agosti 2023 M

# Jarida la UQAB

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Uchomaji Quran na Miitiko ya Kisiasa ya Kinafiki

**HABARI NA MAONI**
Mzigo wa Fedha

**MATOLEO**
India ina Shaka juu ya Mahusiano ya Marekani

**JIBU LA SWALI**
Kumtegemea Dhalimu Kanuni (Qaida) ya la Hafifu katika Maovu Mawili



Afisi ya Habari Tanzania

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿ وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴾

KUMB: 01/1445 Alhamisi, 02 Muharram 1445 H 20/07/2023 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Mwaka Mpya wa Kiislamu Una Ujumbe Mzito wa Kimfumo, na Sio Jambo la Kishereheshereha Tu

Kufuatia kuingia mwaka Mpya wa Kiislamu wa 1445 Hijria ambapo kwa mara ya kwanza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar rasmi imeifanya siku ya tarehe mosi Muharram kuwa siku ya mapumziko, huku Waislamu katika siku hiyo wakifanya amali mbalimbali za kuupokea na kuuadhimisha mwaka huo. Sisi katika Hizb ut Tahrir Tanzania licha ya kushiriki kikamilifu pamoja na Ummah katika baadhi ya amali hizo za kuupokea mwaka huo, tungependa kuweka bayana yafuatayo:

1. Ni kutokana na busara, upeo wa Kiislamu na uoni mpana wa kisiasa ndio uliwafanya Maswahaba (ra) ndani ya mwaka 16 Hijria chini ya Khalifa Umar Khattaab kuwafikiana kwa umoja wao (ijmaa) kuasisi kalenda ya Kiislamu lakini pia kulichagua tukio la ‘Hijra’ kuwa ndio nukta ya kuanzia kuhesabu kalenda hiyo.
2. Uteuzi wa maswahaba wa tukio la ‘Hijra’ kuwa nukta kianzio ya Kalenda ya Kiislamu ni kwa sababu ni kutokana na tukio hilo (Hijra) Waislamu waliweza kuasisi dola yao ya mwanzo ya Kiislamu, wakatoka katika hali ya unyonge na udhalili na kuja katika nguvu/izzah na mamlaka yaliyowawezesha kutekeleza Uislamu kivitendo baada ya kukosa chombo cha kuutekelezea ndani ya Makka kwa kukosa mamlaka. Hivyo, ‘Hijra’ ni mstari uliochora baina ya maisha ya awali ya Waislamu chini ya utawala wa Dar ul Kufr (dola ya kikafiri) ndani ya Makka kuelekea katika maisha matukufu na ya utawala adhimu wa Kiislamu wa Dar ul Islam ndani ya Madina.
3. Uteuzi wa maswahaba wa tukio la ‘Hijra’ walidhamiria kugandisha ufahamu na kutukumbusha mpaka Siku ya Kiama juu jukumu la kuwa na Dola moja ya Kiislamu. Na pale itakapokosekana Umma una uwajibu na jukumu la kufanya ulinganizi, kutafuta Nusra ili kuirejesha tena dola hiyo.
4. Tukio la ‘Hijra’ libebwe ufahamu wake kwa mtazamo ulio sawa na kwa usahihi wake. Lisioneshwe tukio hilo kuwa Mtume (saw) alihama Makka kwa uoga au akawe mkimbizi ndani ya Madina, ukaachwa kando ukweli kuwa Mtume (saw) wakati anafanya ‘Hijra’ tayari alikwishafikia makubaliano na viongozi wa Madina kumpa nusra na kukabidhiwa hatamu za uongozi ndani ya Madina. Hivyo, (Mtume Saw) aliwasili Madina akiwa tayari ni kiongozi aliyetarajiwa kuwasili. Aidha, tukio la ‘Hijra’ lisiangaziwe katika upande mmoja tu wa kimiujiza miujiza kama yaliyojiri katika pango, miujiza kwa Ummu Maabad, Suraqa nk. Hapana shaka miujiza hiyo tunaikubali na kuiamini kwa kuwa ni sehemu ya aqida yetu. Lakini nukta muhimu zaidi ya roho na uhalisia wa ‘Hijra’ ni kuleta mabadiliko ya Kiislamu. Hili ndilo funzo mama na nyeti (la Hijra) ambalo Ummah unastahiki kukumbushwa.
5.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu kuuruzuku Ummah wetu ufahamu sahihi wa tukio hili nyeti na adhimu. Pia Tunamumba aujaalie mwaka huu 1445 Hijria, uwe mwaka wa Nusra na Ushindi kwa kurejeshwa tena Khilafah Rashida kwa Manhaji/njia ya Utume - Amiin

**Masoud Msellem**

**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir Tanzania**

Afisi ya Habari
Denmark

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

KUMB: 01/1445 | Jumanne, 07 Muharram 1445 H | 25/07/2023 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Uchomaji Quran na Miitiko ya Kisiasa ya Kinafiki

Uchomaji moto wa hivi karibuni wa Quran nchini Denmark na Sweden, na miitiko iliyofuata nyumbani na nje ya nchi, inatoa wito wa utambuzi muhimu:

- Uhuru wa kusema ni chombo cha nguvu ya kisiasa na kifuniko duni cha ukosefu wa maadili ya kweli.

- Ni sera endelevu ya kupambana na Uislamu ya serikali mtawalia ambazo zimekuza chuki ya Uislamu katika sehemu za jamii na kuunda mvutano na mgawanyiko kati ya vikundi vya watu.

- Tangu michoro ya kuchukiza iliyoshajiishwa kisiasa, mnamo 2005, serikali ya Denmark imechochea na kuwezesha vitendo vichafu zaidi vya chuki vilivyoelekezwa kwa Waislamu, licha ya athari mbaya kwa jamii.

- Jaribio la serikali lisiloaminika kabisa la kuosha mikono yake kwa "kulaani" kwa Waziri wa Mambo ya nje Lars Løkke Rasmussen, baada ya maandamano makubwa ya ulimwengu, ni la kinafiki na linaloonekana kwa urahisi.

- Hatua na matamko tasa kutoka kwa serikali katika nchi za Waislamu hayana maana. Serikali hizi zinafanya uhalifu dhidi ya Quran mchana na usiku.

- Hatua zinazofaa dhidi ya ukiukwaji huu unaoendelea katika ngazi ya serikali; kidiplomasia, kiuchumi, na ikibidi kijeshi, kamwe hazitaonekana kwa kukosekana kwa nguvu ya kisiasa katika ulimwengu wa Kiislamu ambayo kwa kweli inawakilisha utashi wa Waislamu.

**Elias Lamrabet**

**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir
Denmark**

# HABARI NA MAONI
# Mzigo wa Fedha

**Habari:**

Kenya: Baada ya mswada wa fedha kupitishwa na kutabanniwa na Serikali, sera ya ushuru ilinyanyua kwa kiasi kikubwa wigo wote wa uchumi. Kutabanniwa huku kumezalisha upinzani mkali na hasa wenye utata kuhusu ongezeko la ushuru la 8% kwenye bidhaa za mafuta, ushuru wa nyumba wa 1.5% kwenye mapato, pia ushuru wa 1.5% ya kwa maudhui ya kidijitali na mengi zaidi.

**Maoni:**

Upinzani kutoka kwa Azimio la Umoja na wanaharakati wengine binafsi umeishia tu kupinga kutabanniwa bila ya kuwasilisha badali yoyote, kuashiria kufilisika kwa mfumo wa kibepari katika kuwaondolea watu mzigo huu mkubwa wa fedha. Kwa upande mwengine upinzani wa kisiasa unakosa ikhlasi katika kupigania maslahi ya watu bali unapigania tu umaarufu wa kisiasa pekee.

Utozaji ushuru kama chanzo kikuu cha mapato ya Dola yoyote ya Kibepari unaiacha serikali ya Kenya Kwanza bila chaguo lolote hasa baada ya deni kubwa la taifa kufikia karibu 70% ya Pato la Taifa. Baya zaidi mali zote za umma kama vile umeme, mafuta nk, zinamilikiwa na mashirika ya kibinafsi ambayo lengo lake ni kupata faida kutokana na mateso ya wananchi. Ushuru wa juu na ubinafsishaji wa mali za umma umefanya bili za matumizi ya umma kuwa mzigo wa kifedha bila huruma hata kidogo.

Utozaji ushuru kwa dhati huvunja moyo uzalishaji, suluhu ambayo ubepari ndio huiamini kutokana na uhaba wa rasilimali. Hili linazua swali kwa nini kulitoza ushuru suluhisho la uchumi ambalo ndilo msingi wa riziki? Dosari zilizo katika mfumo huu zinaufanya ushindwe kusimamia mambo ya watu. Kwa nini kutoja ushuru mapato ambayo yamefanyiwa kazi kuchangia Pato la Taifa? Jibu ni rahisi kwamba mali zote za umma zimebinafsishwa na kuwaacha raia chini ya huruma ya mashirika ambayo lengo lao pekee ni FAIDA.

Licha ya kuwa utawala wa Kenya Kwanza unaamini, ukusanyaji mkubwa wa kodi ndio suluhu, matokeo yake ni tofauti na matamshi ya kisiasa kwani ukosefu wa ajira utaongezeka, umaskini utaongezeka pia kushindwa kulipa mikopo pia kutaongezeka kwani mzigo wa fedha utafanya iwe vigumu kwa watu binafsi kulipa deni. Natija yake hili litapelekea kupotosha soko la mitaji kwani wengi wataficha pesa katika akaunti zilizofungwa hadi muda maalum (fixed deposit)  badala ya kuwekeza kwenye soko hilo. Miamala ya kibiashara kama nukta ya uchumi itapungua, wengi watarekebisha matumizi ili kufikia misingi na malipo ya bili kubwa za matumizi.




Uislamu, rehema kutoka kwa Muumba wa mwanadamu, uhai na ulimwengu, unasimama kama uthibitisho wa kihistoria wa jinsi wanadamu walivyoinuliwa kutoka kwenye minyororo ya utumwa wa riba na maumbo ya kisiasa ya zama zao hadi kwenye jamii yenye utendaji wa hali ya juu ambayo iliondoa umaskini na kufanya utafutaji riziki kuwa wenye kupatikana kwa urahisi bila kizuizi kutoka kwa Dola ya Khilafah kwa njia ya Utume lakini badala yake ukawa msahilishaji mkuu wa kufikia riziki yenye heshima.

Mwenyezi Mungu (swt) asema:

مَّا أَفَاءَ اللَّهُ عَلَى رَسُولِهِ مِنْ أَهْلِ الْقُرَى فَلِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ وَلِذِي الْقُرْبَى وَالْيَتَامَى
وَالْمَسَاكِينِ وَابْنِ السَّبِيلِ كَيْ لَا يَكُونَ دُولَةً بَيْنَ الْأَغْنِيَاءِ مِنكُمْ وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ
فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانتَهُوا وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ

**"Mali aliyo leta Mwenyezi Mungu kwa Mtume wake kutoka kwa watu wa hivi vijiji ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na kwa ajili ya Mtume, na jamaa, na mayatima, na masikini, na msafiri, ili yasiwe yakizunguka baina ya matajiri tu miongoni mwenu. Na anacho kupeni Mtume chukueni, na anacho kukatazeni jiepusheni nacho. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu."** [Quran 59:7].

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Ali Omar**
**Mwanachama wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**

# Allahu Akbar... Allahu Akbar... Allahu Akbar



Mwenyezi Mungu ni mkubwa kuliko Mayahudi na ufisadi wao na uadui wao... Mwenyezi Mungu ni mkubwa kuliko Marekani na kiburi chake... Mwenyezi Mungu ni mkubwa kuliko watawala vibaraka wa Waislamu na uatelekezaji na khiyana zao.

Allahu Akbar... Katika siku zilizobarikiwa, damu yetu inamwagika na nyumba zetu zinavunjwa, na watawala wa fedheha hutoa kauli za kukashifu tu.

Allahu Akbar... Je, ni lini ari ya wanaume katika majeshi ya Kiislamu watasonga mbele kuona majeshi yao yakikua katika nyua za Msikiti wa Al-Aqsa?!

Allahu Akbar... Je, jeshi la Misri halina uwezo wa kulitokomeza umbile la Kiyahudi kutoka kwenye mizizi yake katika saa moja ya siku?! Je, jeshi la Jordan halina uwezo wa kuliponda umbile la Kiyahudi na kuliondoa? ... Je, majeshi ya Uturuki na Pakistan hayana uwezo wa kuikomboa Jerusalem na kutimiza ahadi ya Mwenyezi Mungu na bishara njema ya Mtume Wake?!

Allahu Akbar... Je! nafsi zao hazitamani Jihad katika njia ya Mwenyezi Mungu na kuuawa kishahidi katika Ardhi Iliyobarikiwa?!

**Enyi Waislamu:** Mjini Jenin, ardhi ya ushujaa, Mujahidina wachache mashujaa walisimama kidete mbele ya ndege, magari ya kivita, na maelfu ya askari, na hawakuziacha silaha zao, basi vipi kuhusu nyinyi enyi askari wa majeshi ya Kiislamu?!

Uimara wa hawa Mujahidina ulimkasirisha adui yenu, ambapo alitoka akiwa amevaa aibu, na hili linadhihirisha nguvu na dhamira ya waumini katika kukabiliana na maadui zao.

Uimara wa mashujaa hao, licha ya uchache wao na zana zao, unawaanika wazi watawala madhalimu wanaoyafunga minyororo majeshi ya Ummah kutekeleza wajibu wao wa kuunusuru Uislamu na Msikiti wa Al-Aqsa.

Wale waliokasirikiwa wanaunajisi Msikiti wa Al-Aqsa asubuhi na jioni, wanavunja nyumba na kumwaga damu, kisha mtu anatujia akisema tunaionya "Israel" dhidi ya kuvuka mistari mekundu! Unazungumzia mistari gani mekundu?!

Je, kuna mistari mekundu iliyobakia baada ya kuvunjwa nyumba, watu kuhamishwa, kumwaga damu, na kuchafuliwa kwa Msikiti wa Al-Aqsa?!

Ama walio katika nafasi mbaya zaidi ni wale wanaoviomba vyombo vya kimataifa na kuvitaka vitoe ulinzi wa kimataifa, ili Uingereza na Marekani zitoe ulinzi kwa watu wa Palestina?!... Kwa nini msiwahutubie wamiliki wa sababu ili wahamasike kuwalinda watu wa Palestina, au je, ulaji njama na khiyana zinakuzuieni kutafuta msaada wa Umma wa Kiislamu na majeshi yake ili kuikomboa Bayt Al-Maqdis?!

Kwa nini taarifa zote zinatolewa na hotuba zote zinachapishwa na vyombo vya habari vinazifunika kabisa, ama kuhusu hotuba ya kweli ya ukombozi na wito wa Umma wa Kiislamu na majeshi yake, hauna nafasi kwao?! Je, vyombo vya habari vitafikisha ujumbe wetu katika misimamo hii kwa Umma wa Kiislamu na majeshi yake? Au vitafanya ubadhirifu na kuegemea upande wa maadui wa Uislamu ambao hawataki sauti hii ipazwe katika nchi za Kiislamu?!

***Endelea... UK 6***

**Enyi Waislamu:** Kuna njama ya kimataifa na ya kikanda juu ya kuwamaliza Mujahidina katika Ardhi Iliyobarikiwa, na yale yanayotokea mjini Jenin, Nablus na maeneo mengine ni moja ya matunda ya mikutano ya usalama iliyofadhiliwa na Marekani katika kanda hii, ni matunda ya Mkutano muovu wa Aqaba.

Ni makosa ya jinai ya mataifa ya kikanda na Mamlaka ya Palestina, ambayo viongozi wao wanadai kuwa wamesimamisha uratibu wa usalama.

Kwa nini vyombo vya Mamlaka ya Palestina vinaingia katika makao yao makuu, na kila kampeni inayoanzishwa na umbile la Kiyahudi?! Na vipi nafsi za washirika wao zinakubali kudhalilishwa wakiwa wamekaa katika makao yao makuu huku adui akiwauaa ndugu zao na kuzihamisha familia zao?! Wanawezake kujisikia wameridhika kupitia kuwakamata Mujahidina na kuwanyang'anya silaha zao?!

Nchi za Magharibi na za Kiarabu zinawataka watu wa Palestina wajisalimishe kwa umbile la Kiyahudi na kuishi nalo kwa udhalilifu na unyonge. Watawala wetu hawajali Msikiti wa Al-Aqsa, wala hawajali watu wa Palestina. Kwa hiyo, wanaichukulia kila harakati ya mapambano katika Ardhi Iliyobarikiwa kuwa ni harakati inayosumbua usingizi wao na kuamsha ari ya mapambano wanayofanya usiku na mchana kuua nyoyo za Waislamu.

**Enyi Ummah wetu wa Kiislamu:** Sisi kutoka Palestina tunakuhutubieni na kukuambieni, lau watu wa Palestina wangekuwa ndio viongozi, je Ummah ulio hai ungekubali kuvunjwa mkuki wake?! Na ikiwa mashujaa wa Jenin ni watoto wenu, je Ummah utawaangusha watoto wake mashujaa?! Je, usaliti hauadhibiwi kwa kutelekezwa na Mwenyezi Mungu?! Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema:

**مَا مِنَ امْرِئٍ يَخْذُلُ مُسْلِماً فِي مَوْطِنٍ يُنْتَقَصُ فِيهِ مِنْ عِرْضِهِ وَيُنْتَهَكُ فِيهِ مِنْ حُرْمَتِهِ إِلَّا خَذَلَهُ اللهُ فِي مَوْطِنٍ يُحِبُّ فِيهِ نُصْرَتَهُ وَمَا مِنْ أَحَدٍ يَنْصُرُ مُسْلِماً فِي مَوْطِنٍ يُنْتَقَصُ فِيهِ مِنْ عِرْضِهِ وَيُنْتَهَكُ فِيهِ مِنْ حُرْمَتِهِ إِلَّا نَصَرَهُ اللهُ فِي مَوْطِنٍ يُحِبُّ فِيهِ نُصْرَتَهُ**

**"Hakuna mtu (Muislamu) atakayemtelekeza Muislamu mahali ambapo heshima yake inatwezwa na utukufu wake unadunishwa bila ya Mwenyezi Mungu naye kumtelekeza mahali anapotaka msaada wake; na hakuna mtu (Muislamu) ambaye atamsaidia Muislamu mahali ambapo heshima yake inatwezwa na utukufu wake kuvunjwa bila ya Mwenyezi Mungu kumsaidia mahali anapotaka msaada wake."** (Imesimuliwa na al-Tabarani kwa isnad hasan).

Je, mutaiacha Aqsa yenu na Masrah yenu, watoto wenu na ndugu zenu katika Dini na imani chini ya mashambulizi ya umbile la Kiyahudi na uhalifu na dhulma yao huku mkitazama tu?!

**Enyi Watu wa Ardhi Iliyobarikiwa:** vumilieni, na mustahamili; kuweni wamoja, na mtakuwa watukufu kwa imani yenu na uthabiti wenu, na ugeukieni Ummah wenu na mtafute msaada wake kwa ajili ya ushindi wenu, na kuwa kichocheo cha mwamko wake na chanzo cha izza. Itegemeeni Dini yenu na Ummah wenu, mtegemeeni Mola wenu, Ambaye mkononi Mwake uko ushindi wenu pekee, na achaneni na miradi ya usaliti na tawala vibaraka, wala msikate tamaa na faraja ya Mwenyezi Mungu.

**إِنَّهُ لَا يَيْأَسُ مِنْ رَوْحِ اللَّهِ إِلَّا الْقَوْمُ الْكَافِرُونَ** **"Hakika hawakati tamaa na faraji ya Mwenyezi Mungu isipo kuwa watu makafiri."** [Yusuf 12:87]. Msikate tamaa na Ummah wenu kwani wao ndio asili ya mashujaa na wanaume, kwani miito ya Ardhi iliyobarikiwa inayotafuta msaada (Nusrah) ya Umma wa Kiislamu na majeshi yake ili kusimamisha Khilafah na kuikomboa Ardhi iliyobarikiwa, Mwenyezi Mungu atawatolea njia ya kuzifikia nyoyo za Waislamu, ambapo nyoyo zinazotamani Siku ya Ushindi na Tamkini zitawasikiliza. Msiache kuwalingania kwa maneno ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:

**يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا مَا لَكُمْ إِذَا قِيلَ لَكُمُ انْفِرُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ اثَّاقَلْتُمْ إِلَى الْأَرْضِ أَرَضِيتُمْ بِالْحَيَاةِ الدُّنْيَا مِنَ الْآخِرَةِ فَمَا مَتَاعُ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا فِي الْآخِرَةِ إِلَّا قَلِيلٌ * إِلَّا تَنْفِرُوا يُعَذِّبْكُمْ عَذَاباً أَلِيماً وَيَسْتَبْدِلْ قَوْماً غَيْرَكُمْ وَلَا تَضُرُّوهُ شَيْئاً وَاللَّهُ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ**

**"Enyi mlio amini! Mna nini mnapo ambiwa: Nendeni katika Njia ya Mwenyezi Mungu, mnajitia uzito katika ardhi? Je, mmeridhia maisha ya dunia kuliko ya Akhera? Lakini starehe za maisha ya dunia kulinganisha na ya Akhera ni chache. Kama hamwendi atakuadhibuni adhabu chungu, na atawaleta watu wengine, wala nyinyi hamtamdhuru chochote. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu."** [At-Tawbah 9:38-39]. Kuhamasika kwa majeshi ya Ummah na kukombolewa kwa Bayt Al-Maqdis kutatokea, Mwenyezi Mungu akipenda, hiyo ni ahadi ya dhati.

Ewe Mwenyezi Mungu tufikishie kheri hii kwa niaba yetu na uzifungue nyoyo za Waislamu kwa yaliyomo ndani yake ya kheri na hekima, na utupe kiongozi mshindi kutoka Kwako, Ewe Mwenyezi Mungu, wapokee mashahidi wetu na uwaponye majeruhi wetu, na tupate ushindi wako uliotuahidi.

Ewe Mwenyezi Mungu, waadhibu wale waliokasirikiwa na Mwenyezi Mungu na wale waliokula njama nao. Ewe Mwenyezi Mungu, yajaalie maangamizo yao katika usimamizi wao, na udanganyifu wao dhidi yao, na ulinde Ummah wetu na Dini yetu, na utujaalie tuwe miongoni mwa wale uliowachagua ili kuisimamisha Dini Yako na kunyanyua hadhi ya wito wako. Alhamdulillah Rabb Al Alamin.

| | |
|---|---|
| H. 17 Dhu al-Hijjah 1444 | Hizb-ut-Tahrir |
| M. Jumatano, 05 Julai 2023 | Ardhi ya Baraka-Palestine |

# India ina Shaka juu ya Mahusiano ya Marekani

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Adnan Khan**



Marekani iliondoa vizuizi vyote wakati Waziri Mkuu wa India Narendra Modi alipozuru Marekani mwishoni mwa Juni katika ziara rasmi ya kiserikali. Modi, ambaye wakati fulani alinyimwa visa ya kusafiri kwenda Marekani kwa sababu ya wasiwasi juu ya haki za binadamu, alikula na kulala katika Ikulu ya White House na hata kuhutubia kikao cha pamoja cha Bunge la Congress. Marekani imetamani uhusiano wa kina na wa kimkakati na India tangu kugawanyika, ambao umechukua umuhimu zaidi na kukua kwa China. Lakini uhusiano kati ya Marekani na India haujafikia uwezo wake huku New Delhi ikiendelea kuwa na mashaka mbalimbali.

Wakati Marekani ilipoibuka kuwa dola kuu yenye nguvu duniani baada ya Vita vya Pili vya Dunia na Vita Baridi vilipokuwa vikianza, huko Asia Kusini watunga sera wa Marekani walikuja kuiona India kama dola yenye nguvu katika eneo hilo na taifa muhimu mno ambalo Marekani ililihitaji ili kuzuia kuenea kwa ukomunisti. Lakini waanzilishi wa India hawakutaka kuchukua upande katika Vita Baridi na walitafuta mahusiano mazuri na Marekani na Muungano wa Kisoviet. Wote wawili Gandhi na Nehru walitazamia India ambayo ilikuwa ya kisekula na iliyofuata muangaza wa mawazo ya Ulaya, huku katika uchumi walivutiwa na mtindo wa Kisoviet, na walitafakari mahusiano ya kina ya kiuchumi nao. Katika sera ya kigeni waanzilishi walijificha nyuma ya kutofungamana na mtu ili wasichukue upande katika Vita Baridi.

Kutokana na hali hiyo Marekani ililazimika kukaa na Pakistan kama mshirika wake katika eneo hilo ambaye kisha alijiunga na mashirika ya Vita Baridi yaliyoongozwa na Marekani na kupokea misaada na vifaa vya kijeshi vya Marekani. Maafisa wa Marekani hata hivyo waliendelea kuwasiliana na India ili kupata imani yake na kuiunganisha katika muundo wa muungano wake wa Vita Baridi. Wakati India ilipopigana vita na China huko Himalaya mnamo 1962 Marekani ilipeleka silaha India ili kuisaidia juhudi zake za vita.

Wakati Muungano wa Kisovieti ulipoporomoka mwaka wa 1991, mshirika mkuu wa kibiashara wa India sasa alikuwa ametoweka jambo ambalo lilisababisha mgogoro wa kiuchumi, ambao uliilazimisha New Delhi kugeukia IMF. Kutokana na masharti ya IMF yaliyohitaji ukombozi na hitaji la India la mtaji na uwekezaji katika miaka ya 1990, India ilipitia msukumo mkubwa wa ukombozi. Katika mgao wa amani baada ya kumalizika kwa Vita Baridi watunga sera wa Marekani waliona fursa mpya ya kujishindia India.

***Endelea... UK 8***

Kwa kukua kwa China katika miaka ya 2000, umuhimu wa India ukawa wa dharura zaidi kwa Marekani. Mnamo 2005, Waziri wa Mambo ya Nje wa wakati huo wa Marekani Condoleezza Rice alisema kwamba kuisaidia India kuwa dola ya kimataifa lilikuwa ni lengo la sera ya Marekani. Kufikia mwaka wa 2006, Bunge la Congress la Marekani lilipitisha Mkataba wa kihistoria wa Nyuklia wa India-Marekani ambao ulifungua njia ya kuhamisha teknolojia ya nyuklia ya kiraia hadi India. Hii pia iliondoa vikwazo vyote vya Marekani kwa India baada ya majaribio ya nyuklia ya 1998.

Lakini licha ya msukumo wa Marekani wa kusawazisha mahusiano na India, kumekuwa na changamoto nyingi. India na Marekani hazina makubaliano ya biashara huria kati yao. Kampuni za Marekani kwa muda mrefu zimekuwa zikitaka ufikiaji wa soko kubwa la ndani la India na tawala mtawalia jijini New Delhi zimelinda soko la ndani kwa sera za ulinzi. Lalamiko kuu la Marekani dhidi ya India ni matumizi yake ya vikwazo vya ushuru na visivyo vya ushuru kuwakinga wazalishaji wa kilimo na kuchagua viwanda vya utengenezaji.


Lakini pamoja na matatizo haya Marekani imefanya katika miaka ya hivi karibuni mikataba mingi ya kiuchumi ambayo ilitarajia itafungua njia ya uhusiano wa kina. Marekani imesema inapanga kutoa ufadhili kwa ajili ya kuanza kwa teknolojia ya India na miradi ya miundombinu kutoka kwa Mfuko wake wa Ushirikiano wa Kimataifa wa Miundombinu na Uwekezaji (PGII) wenye thamani ya dolari bilioni 200. Mnamo Januari 2023 washauri wa usalama wa kitaifa wa India na Marekani walitangaza kuzinduliwa kwa Mpango wa Marekani-India katika Teknolojia Muhimu Zinazoibuka (iCET). Ushirikiano huu wa kimkakati wa teknolojia ni dhahiri unahusiana na wasiwasi wa Marekani kuhusu China, ambayo India inaonekana kushiriki pamoja nayo. Lakini inabakia kuonekana endapo India itaunganisha teknolojia zake na zile za Marekani na kuachana kabisa na teknolojia ya China na Urusi.

Modi anapotembelea India, hatimaye Marekani iko mahali ambapo imeimarisha mahusiano na India, baada ya miongo kadhaa ya kuachwa kwenye baridi. Lakini uhusiano huu, licha ya makubaliano yote ya kiuchumi na kijeshi, sio muungano na bado unakabiliwa na shida nyingi. India haiuoni ulimwengu kama Marekani inavyouona. Kwa muda mrefu, kikwazo kikubwa kwa uhusiano wa karibu wa India na Marekani ni kwamba nchi zote mbili zina historia ya kuwa na urafiki na wapinzani wa kila mmoja. India inachukia kuendelea kwa usaidizi wa kimada wa Marekani kwa Pakistan. Pia ina shaka na majaribio ya sasa ya Marekani ya kudhibiti na kushirikiana na China kwa wakati mmoja. Ingawa India ina mzozo wa mpaka na China pia ina mahusiano ya kiuchumi nayo na inataka haya yaendelee. India haiangalii China jinsi Marekani inavyoiangalia. India kwa kweli haiyaoni mambo mengi jinsi Marekani inavyoyaona, lakini inataka kufaidika na uwekezaji, teknolojia na biashara ya Marekani.

Watawala wa India kihistoria hawajawa vibaraka wa Marekani mithili ya watawala wengi wa Waislamu walivyofanya. Wengi wa watawala wa Waislamu ima walijiunga na Marekani kwa manufaa yao binafsi au waliletwa madarakani na Marekani. Wanahalalisha uwepo wa Marekani na kuendeleza umuhimu wake, huku mataifa mengine yakiuona uhalisia wa Marekani na yana shaka kuiunga mkono.

JIBU LA SWALI

# Kumtegemea Dhalimu Kanuni (Qaida) ya la Hafifu katika Maovu Mawili



**Swali:**

Assalam Alaikum Wa Rahmatullah Wa Barakatuh

Awali ya yote napenda kukushukuru na kukusifu kwa juhudi zako zilizobarikiwa, na namuomba Mwenyezi Mungu (swt) akunusuru kwa ushindi wake, na aandae kwa ajili ya ulinganizi huu wenye kuunusuru kama Saad bin Muadh, na tunamuomba kwa hilo uuondolee ugumu Ummah, na kuurudisha katika zama zake za awali.

Nina maswali mawili muhimu, na natumai kuwa jibu litakuwa la kina kadiri inavyowezekana, nikijua kuwa majibu yanayochapishwa ni ya kina kila wakati, lakini ningependa dalili nyingi za Shariah zenye maelezo ya kina ili ufahamu wa maswala haya uwe wa kina. Ama kuhusu swali langu:

**La kwanza**, kwa nini hairuhusiwi kumtegemea dhalimu (au mtu yeyote ambaye ana mamlaka na ushawishi na ana uwezo wenye manufaa, awe ni mnafiki, mtenda dhambi au hata kafiri) kwa kumuomba pesa au msaada ili Muislamu anaweza kupigana jihad, au hata kuinusuru Dini?

La Pili, ikiwa uko katika nchi, watu wake wengi ni Waislamu, na kuna uchaguzi wa urais. Wagombea wote hawataki kutawala kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu isipokuwa mmoja anayetaka kutawala kwa baadhi ya yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, huku ukijua kwamba mgombea huyu atahifadhi baadhi ya madhihirisho ya Kiislamu. Wagombea wengine wanaweza kuwahamisha baadhi ya wakaazi wa nchi hiyo na kuharibu madhihirisho mengi ya Uislamu, na wataeneza maovu na maadili machafu. Basi je, inajuzu kwangu kwa mujibu wa Shariah kumchagua muovu mdogo miongoni mwao, kama msemo maarufu unavyosema: (msiba ni mdogo kuliko msiba) na wakati huo huo Waislamu hawana uwezo wa kusimamisha udhalilifu huu na ni uhalisia uliolazimishwa. Kwa hiyo, nikimruhusu muovu (kiongozi) atawale, atawafanya watu wahamishwe na anaweza kuwachinja ndugu zangu Waislamu, na lau nitampa kura yangu yule muovu mdogo, basi nitakuwa nimekubali kutawaliwa na mtu asiyetaka kutawala kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu.

**Jibu:**

Wa Alaikum Assalam Wa Rahmatullah Wa Barakatuh,

**Kwanza: Kuhusu swali lako la kwanza, jibu liko katika swali hilo:**

1- Unauliza [Kwa nini hairuhusiwi kumtegemea dhalimu (au mtu yeyote ambaye ana mamlaka na ushawishi na ana uwezo wenye manufaa, awe ni mnafiki, au mtenda dhambi, au hata Kafiri), kwa kumuomba pesa au msaada ili Muislamu apigane jihad, au hata kuinusuru Dini?], kana kwamba unakusudia kwa kauli yako (kumtegemea dhalimu) kauli yake Mtukufu:

***Endelea... UK 10***

وَلَا تَرْكَنُوا إِلَى الَّذِينَ ظَلَمُوا فَتَمَسَّكُمُ النَّارُ وَمَا لَكُمْ مِنْ دُونِ اللهِ مِنْ أَوْلِيَاءَ ثُمَّ لَا تُنْصَرُونَ

**"Wala msiwategemee wanao dhulumu, usije ukakuguseni Moto. Wala nyinyi hamna walinzi badala ya Mwenyezi Mungu, wala tena hamtasaidiwa."** [Hud: 113] Imebainika kutokana na Aya hii kwamba uregee kwenye uharamu wa kuwategemea wale waliodhulumu, basi vipi unauliza juu ya kujuzu kwake?

2- Yafuatayo yameelezwa katika tafsiri ya Al-Qurtubi ya Aya hii:

[...Ina maswala manne: la kwanza – Kauli yake: (Wala **msiwategemee**) uhalisia wa kuegemea ni kutegemea, kuegemea, kujiliwaza na jambo na kutosheka nalo. Qatada akasema: Maana yake usiwe na urafiki nao na usiwatii. Ibn Jurayj (alisema): Usiegemee kwao. Abu Al-Aaliya (alisema): Msitosheke na matendo yao, na wote wanakaribiana...

Tatu - kauli ya Mwenyezi Mungu:

إِلَى الَّذِينَ ظَلَمُوا

**"wanao dhulumu"** ikasemwa: watu wa shirki. Na ikasemwa: Ni jumla kuhusu wao na kuwaasi kwao, kama katika kauli ya Mwenyezi Mungu:

وَإِذَا رَأَيْتَ الَّذِينَ يَخُوضُونَ فِي آيَاتِنَا

**"Na unapo waona wanao ziingilia Aya zetu"** [Al-An'am: 68] Hili lilielezwa hapo awali. Na hili ni sahihi katika maana ya Aya. Inaashiria kuachana na makafiri na kutowatii watu wa bid'a na wengineo. Kusuhubiana nao ni Ukafiri au uasi, kwa sababu usuhuba hupatikana tu kutokana na mapenzi.

Nne - kauli yake Mwenyezi Mungu:

فَتَمَسَّكُمُ النَّارُ

**"ukakuguseni Moto"** yaani itakuunguzeni; kwa kuchanganyika nao, kusuhubiana nao, kufuata pingamizi zao, na kuafikiana nao katika mambo yao...] Mwisho.

**Imebainika kutokana na tafsiri ya Aya hii kwamba kumtegemea dhalimu ni haramu kabisa, na hakuna shaka juu yake, iwapo dhalimu ni kafiri au Muislamu muasi. Kwa hivyo, kumtegemea dhalimu kupitia mapenzi yake, utiifu, mwelekeo kwake, kumtegemea, kumsifu, na kukaa kimya juu ya udhalimu wake ... nk, yote yanakuja chini ya kutegemea, ambako ni haramu kutokana na andiko la ayah tukufu.**

3- Pia kwa mujibu wa swali lako, dhalimu anaweza kuwa mtawala kafiri, na anaweza kuwa mtawala muasi au mnafiki anayetawala kwa yasiyokuwa Uislamu, kama ilivyo kwa watawala wa Waislamu leo.

a- Iwapo mtawala ni kafiri, basi kuomba msaada kwake haijuzu kwa mujibu wa Shariah, hata ikiwa ni kwa kuchukua pesa kutoka kwake kufanya jihad kwa sababu kuchukua pesa kutoka kwake bila shaka kunapelekea kumpa mamlaka juu ya upande uliochukua pesa kutoka kwake, ambayo ni mandhari yakuhisika, haswa linapokuja suala la makundi yanayopigana na wanamgambo. Wanakuwa ni mateka wa nchi zinazowafadhili, na maamuzi yao hayana thamani yoyote, kwa sababu yeyote aliye na ufahamu mdogo wa ukweli wa mambo anatambua kuwa nchi hazitoi msaada wa hisani, hivyo pesa zote ambazo nchi yoyote duniani inatoa upande mwengine usiokuwa wananchi wake ni kufikia malengo fulani kwa ajili yake, na haijali maslahi ya upande inayotoa misaada. Pindi watu binafsi, makundi na mapote yanapochukua pesa kutoka kwa nchi za kigeni, za makafiri kwa ajili ya jihad na kupigana na mvamizi, kwa yakini huo ni ushirikiano na mgeni na kujiua kisiasa, na huwapa makafiri mamlaka juu ya Waislamu, na Mwenyezi Mungu (swt) asema:

وَلَنْ يَجْعَلَ اللهُ لِلْكَافِرِينَ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ سَبِيلاً

**"…wala Mwenyezi Mungu hatawapa makafiri njia ya kuwashinda Waumini."** [An-Nisa: 141]

b- Lakini ikiwa mtawala ni muasi, kama hali halisi ya watawala wa sasa katika nchi za Kiislamu, yeye pia haitoi pesa kwa upande wowote wa nje isipokuwa kufikia malengo fulani, na mara nyingi malengo haya ni ndani ya mipango inayotolewa na nchi za makafiri kwa sababu watawala wa Waislamu ni vibaraka wa nchi za kikoloni za makafiri. Kwa hiyo, upande ambao inafungamana na mtawala yeyote katika nchi za Kiislamu na kupata usaidizi na uungwaji mkono kutoka kwake huwa ni chombo mikononi mwa mtawala huyo anayekielekeza apendavyo. Tuliyoyaona huko Ash-Sham hayako mbali na sisi, katika suala la utegemezi wa makundi na mashirika mengi juu ya pesa chafu za kisiasa ambazo nchi za eneo hilo zinawapa, bila kusahau sifa zinazoelekezwa na pande zinazohusishwa na watawala madhalimu na utiifu wao, kung'arisha sura zao na kutozikataa... n.k hayo yote bila shaka yameharamishwa vile vile kwa sababu yanapelekea kupuuza haki na malengo ya Waislamu na kumfanya mchukuaji pesa kuwa mtumishi wa dhalimu na msaliti kwa Ummah wake na Dini yake.

4- Zaidi ya hayo, jihad katika njia ya Mwenyezi Mungu (swt) na kuinusuru Dini sio kwa kutafuta msaada wa makafiri au watawala madhalimu, kwa sababu makafiri ni maadui wa Waislamu na wao ndio ambao Ummah lazima unapaswa uwapige vita na kukabiliana nao. Haiingii akilini kwamba jihad yao ni kwa kuchukua misaada na pesa kutoka kwao, kwani huu ni mgongano wa wazi. Bali jihad na kunusuru Dini ni kwa kuutegemea Ummah na kuufanya kuwa ndio chanzo cha nguvu na utoaji.

***Endelea... UK 11***

Zaidi ya hayo, watawala madhalimu katika nchi za Kiislamu ni zana mikononi mwa makafiri, basi vipi itadhaniwa kuwa Muislamu atachukua misaada na pesa kutoka kwao ili kuwapiga vita makafiri na kuinusuru Dini, maadamu wao ni zana duni mikononi mwa makafiri, maadui wa Ummah, na wanausibu Ummah kwa adhabu kali kabisa, na kupigana na mujahidina wakweli na wabebaji Dawah wakweli?!

**Pili: Ama kuhusu swali lako la pili:**

**Tayari tulishajibu kwa kina mnamo tarehe 29/8/2010, kuhusu kanuni ya la hafifu katika maovu mawili (au kama unavyosema katika swali lako:** (msiba ni mdogo kuliko msiba)**, na haya ndio maandishi yake:**

[Kanuni: “La Hafifu katika Maovu Mawili au La Hafifu katika Madhara Mawili” Hii ni kanuni ya Shariah iliyotabanniwa na wanazuoni wa fiqhi wengi. Na kwa mujibu wa wanavyuoni wanaoitabanni, ina maana moja ambayo ni kuruhusiwa kufanya mojawapo ya matendo mawili yaliyoharamishwa, ni kipi katika vitendo viwili chenye uharamu mdogo **endapo mtu aliyekalifishwa na Mwenyezi Mungu (Al-Mukalaf) hana budi ila kufanya moja kati ya mawili yaliyoharamishwa na hawezi kujiepusha nayo, kwa sababu ni nje ya uwezo wake kwa kila njia.** Mwenyezi Mungu (swt) asema:

لَا يُكَلِّفُ اللَّهُ نَفْساً إِلَّا وُسْعَهَا

**“Mwenyezi Mungu haikalifishi nafsi yoyote ila kwa kadiri ya iwezavyo.”** [Al-Baqara: 286]. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

فَاتَّقُوا اللَّهَ مَا اسْتَطَعْتُمْ

**“Basi mcheni Mwenyezi Mungu kama mwezavyo”** [At-Taghabun: 16].

Yaani, kanuni hii kwa mujibu wa walioitabanni inatumika tu ikiwa hakuna njia ya kuepuka kufanya mojawapo ya makatazo mawili, wakati huwezi kuachana na matendo yote mawili yaliyoharamishwa isipokuwa kufanya kitendo kikubwa zaidi kilichoharamishwa, basi dogo la maovu mawili linachukuliwa. Wanachuoni hawa pia hawafafanui la hafifu katika maovu mawili kwa mujibu wa matamanio, bali kwa mujibu wa hukmu za Shariah. Kwa mfano, ulinzi wa nafsi mbili unatangulizwa kuliko kuhifadhi nafsi moja, na kuhifadhi nafsi tatu ni bora zaidi, na kadhalika. Kuhifadhi nafsi kunakuja kabla ya kuhifadhi mali. Kuihifadhi Dar ul Islam kunakuja chini ya kuhifadhi Dini ambayo ni muhimu zaidi kuliko kuhifadhi roho na mali. Kadhalika, Jihad na utawala (Imamah) mtukufu yako chini ya kuhifadhi Dini ambayo ni ya juu na muhimu zaidi ya mahitaji. Mwanachuoni Ash-Shatibi amesema katika Al-Muwafaqat: “Nafsi zinaheshimiwa na kuhifadhiwa na lazima ziokolewe, ikiwa kuna chaguo kati ya kuiruhusu nafsi kuishi au kupoteza mali juu yake, au kuiua nafsi na kuhifadhi mali, basi kuiweka nafsi hai kunatangulizwa.”

Mifano iliyotajwa na wanazuoni hawa katika matumizi ya kanuni hii ni pamoja na:

1- Iwapo mwanamke anakabiliwa na hatari katika uchungu wa uzazi na ikawa vigumu kuwaokoa mama na mtoto na uamuzi wa haraka unahitajika: ima kumwokoa mama ambayo inapelekea kifo cha mtoto, au kumuokoa mtoto ambaye ni kifo cha mama, na ikiwa hali hiyo itaachwa na mmoja wa hao wawili akatolewa muhanga ili kuokoa mwingine au mmoja kuokolewa na kifo cha mwingine, hii inaweza kusababisha kifo cha wote wawili. Katika hali hii tunaweza kutumia “la hafifu katika maovu mawili, haramu mbili, au madhara mawili, ambayo ni kutekeleza kitendo cha kumwokoa yule anayetakiwa katika kesi hii, ambaye ni mama, hata kama kitendo hiki hiki kitamuua wa pili.

2- Kwamba mtu anazama maji au kuuwawa na mtu mwingine, au kudhuriwa sana mwilini na viungo vyake, au mwanamke kunajisiwa, mbele ya mtu aliyekalifishwa na Mwenyezi Mungu (Mukalaf) ambaye anaweza kuzuia maovu haya na ana swala ya faradhi ambayo huenda ikampita wakati wake; ima azuie kitendo hicho kilichoharamishwa na akose kutekeleza wajibu, au akiwa atatekeleza wajibu kwa wakati, basi kitendo hicho kilichoharamishwa kitatendeka, na muda hautoshi wa kufanya mambo yote mawili kwa pamoja. Hapa yanakuja matumizi ya kanuni hii, na mizani pia inaamuliwa na Shariah, ambayo ilifanya kuondolewa kwa makatazo haya yaliyotajwa hapo juu kuwa ya kutangulizwa kuliko kutekeleza jukumu lililotajwa hapo awali, lakini ikiwa inawezekana kutekeleza majukumu yote mawili kwa pamoja, basi hilo linakuwa wajibu.

3- Hii ni mifano mengine iliyotajwa na Imam al-Ghazali na Izz al-Din ibn Abd al-Salam, Mwenyezi Mungu awarehemu, inayoonyesha matumizi ya kanuni ya “la hafifu katika maovu mawili”, kwa mujibu wao, na pia kuonyesha mizani kati ya hukmu. Al-Ezz amesema katika kitabu chake “Qawa’id Al-Ahkam Fi Masalih Al-Anam”: “Ikiwa uovu mtupu utaungana, endapo inawezekana kuuzuia, tutauzuia. Ikiwa ni vigumu kuzuia maovu yote, tunazuia lenye kudhuru zaidi na kufuatiwa na lenye kudhuru zaidi na baya na baya zaidi,” kwamba mtu analazimishwa kumuua Muislamu, na akikataa maana yake ni kwamba atauawa, hivyo basi ni lazima aepuke madhara ya kumuua (Muislamu) kwa kuwa na subira ya kuuwawa, kwa sababu subira yake ya kuuwawa haina madhara kuliko kumuua (Muislamu) ...” Huu ni mfano wa wazi kwamba ni chaguo kwa la hafifu katika madhara mawili au haramu mbili, kwa sababu hawezi kuepuka yote mawili, na ikiwa anaweza kuzuia madhara mawili, ni lazima afanye hivyo.

Na amesema katika mfano mwingine: “Kadhalika, akilazimishwa kumuua mtu kwa kutoa ushahidi wa uongo au hukmu ya uongo (dhidi ya Muislamu), au atauwawa. Ikiwa yule anayelazimishwa kutoa ushahidi au kutoa hukmu inayopelekea kuuwawa mtu, au kumkatakata,

***Endelea... UK 12***

au kufanya Zina, ushahidi au hukmu hiyo haijuzu, kwa sababu kujisalimisha kwa kuuwawa kunatangulizwa kuliko kusababisha kuuwawa Muislamu asiye na dhambi, au kumkatakata bila kosa, au kutenda Zina...", yaani ikiwa atauwawa au kutoa ushahidi wa uongo dhidi ya mwingine ambao unapelekea kumuua au kumkatakata, au kumshambulia heshima yake, basi haijuzu kwake kushuhudia bali awe na subira ya kuuwawa, kwa sababu kusalimu amri kwa kuuwawa kwake kunatangulizwa kuliko kumuua Muislamu mwingine.

Kwa maana nyengine, hali ya mtu anapokimbilia kutekeleza la hafifi ya makatazo mawili au madhara mawili ni pale mtu anaposhindwa kuepuka au kuzuia mambo yote mawili yaliyoharamishwa.

Hii ni mifano ya matumizi ya kanuni ya "la hafifu katika maovu mawili", kulingana na wale wanachuoni wanaoitabanni. Hata hivyo, yale ambayo 'wanazuoni wa serikali' wanayapigia debe au wale wanaotaka Muislamu kuzipa mgongo hukmu za Shariah kwa kupotosha na batili hayatoki katika mifano ya kanuni hii.

Wale wanaotumia kanuni hii kufanya kitendo hiki kilichoharamishwa badala ya kitendo kile kilichoharamishwa, wakihalalisha matendo yao kwa kuogopa kufungwa au kufutwa kazi, huu sio mfano wa kanuni hii.

Kadhalika wale wanaosema tunashiriki katika utawala wa kikafiri ijapokuwa imeharamishwa, ili tusiwaachie wapotovu vyeo vyote vya kutawala kwani kuwaachia ni haramu zaidi... hili sio miongoni mwa matumizi ya kanuni hiyo, badala yake ni kama mtu anayesema tunafungua baa (kwa ajili ya pombe) na kupata pesa kutoka kwayo badala ya kumwacha kafiri aifungue na kupata pesa.

Sio miongoni mwa matumizi ya kanuni kwamba mtu anawasilishwa na mambo mawili yaliyoharamishwa na anachagua dogo wakati ana uwezo wa kujiepusha na yote mawili, kama vile kusema wale wanaosema mchague fulani, hata kama yeye ni kafiri mkisekula au fasiki, au muunge mkono fulani na wala usimuunge mkono mwengine, kwa sababu wa kwanza anatusaidia na wa pili hautusaidii, au mithili kitu kama hicho, bali yale yanayosemwa hapa: masuala haya mawili yaliyowasilishwa mbele yetu yameharamishwa, kwa hivyo haijuzu kumchagua mtu wa kisekula na haijuzu kumteua kuwa mjumbe kumwakilisha Muislamu katika rai, kwa sababu hashikamani na Uislamu, na kwa sababu anafanya vitendo vilivyoharamishwa ambavyo haviruhusiwi kwa mjumbe kutekeleza kama kutunga sheria na kuidhinisha miradi iliyoharamishwa, na kulingania vitu vilivyo haramishwa, kuvikubali na kuvifuata, yaani anakataza mema na kuamrisha maovu. Kwa hiyo, hakuna hata mmoja wao anayepaswa kuchaguliwa; kwa sababu kumchagua yeyote kati yao ni haramu. Na kujiepusha na uchaguzi wa yeyote kati yao iko ndani ya uwezo wa mtu.

Sio mojawapo ya matumizi ya "la hafifu katika maovu mawili" kwamba Muislamu anakabiliana na vitendo viwili vilivyoharamishwa, na anaweza kujiepusha na vyote viwili, lakini anachagua lililo jepesi zaidi kulingana na matamanio yake, na analitekeleza kwa madai kuwa ni vigumu kuzuia haramu zote mbili…! Bali ni lazima ajiepushe na makatazo yote maadamu hilo linawezekana kwake kwa mujibu wa hukmu za Shariah.

Hii ni picha fupi ya "la hafifu katika ya maovu mawili" au "la hafifu katika madhara mawili"] Mwisho wa kunukuu jibu la swali lililotangulia.

Natumai hili linatosheleza, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Zaidi na Mwenye Hekima.

**Ndugu Yenu,**

**Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah**

**23 Dhul Hijjah 1444 H**
**11/7/2023 M**